

# Google Chat

## Google Ireland Limited (“Google”)

Gordon House, Barrow Street, Dublin 4, Ireland

<https://support.google.com/>

*Itanza Kutumika Tarehe 21 Disemba, 2020*

### Muhtasari wa Mkataba

- Muhtasari huu wa mkataba unafafanua vipengee muhimu vya huduma tunayoitoa kulingana na matakwa ya sheria ya Umoja wa Ulaya<sup>1</sup>.
- Dhamira yake ni kukusaidia kulinganisha huduma mbalimbali zinazotolewa.
- Maelezo kamili kuhusu huduma tunayoitoa yanapatikana katika hati nyingine.

### Huduma

Google Chat ni huduma ya kutuma ujumbe papo hapo inayotolewa katika vifaa na mifumo mbalimbali kupitia kiolesura cha wavuti au programu. Muunganisho wa intaneti unahitajika ili kutuma au kupokea ujumbe kupitia Google Chat. Google Chat inatolewa na Google kwa kutumia ustadi na umakini unaofaa, ingawa viwango vya chini zaidi vya ubora wa huduma zinazotolewa havijabainishwa.

### Bei

Google Chat inatolewa bila malipo na matumizi yake yanapaswa kutii Sheria na Masharti ya Google (yanayopatikana <https://policies.google.com/terms>).

### Muda, usasishaji na utamatishaji

Unaweza kupata na kutumia Google Chat mara tu baada ya kujiisajili. Hulazimiki kutumia Google Chat kwa muda fulani uliobainishwa na uko huru kuacha kuitumia wakati wowote.

### Vipengele kwa ajili ya watumiaji walio na ulemavu

Unaweza kutumia vijibu kama sehemu ya Google Chat kusaidia kufanya kazi kiotomatiki na pia kutumia visoma skrini na mikato ya kibodi. Maelezo zaidi yanapatikana <https://www.google.com/accessibility/>.

### Maelezo mengine muhimu

Usaidizi kwa Wateja: Usaidizi kuhusu Google Chat unapatikana <https://support.google.com/>.

Migogoro: Unaweza kupeleka malalamiko kwa mtoa huduma mbadala wa kutatua migogoro aliyerodheshwa <https://ec.europa.eu/consumers/odr/main/?event=main.adr.show2> au mtoa huduma mwingine, kama inavyohitajika na sheria za nchi yako. Maelezo zaidi yanapatikana kwenye Sheria na Masharti ya Google.

Matukio ya Usalama: Google ina mpango wa kina wa udhibiti wa matukio ya kila siku, usiku na mchana ili kutambua na kuitikia matukio ya usalama au ya faragha bila kuchelewa. Google pia inatoa Orodha ya Masuala ya Usalama ya kukagua ili kukusaidia kudhibiti usalama wako mtandaoni.

Data Binafsi: Ili ujisajili kwenye Google Chat, unahitaji kutoa jina, anwani ya barua pepe na nambari yako ya simu. Sera ya Faragha ya Google (inayopatikana <https://policies.google.com/privacy>) inatoa maelezo zaidi kuhusu data binafsi ambayo Google hukusanya unapotumia Google Chat. Sera ya Faragha ya Google si sehemu ya mkataba kati yako na Google wala si sehemu ya muhtasari huu.

---

<sup>1</sup> Ibara ya 102(3) ya Agizo (EU) 2018/1972 la Bunge la Ulaya na la Baraza la Tarehe 11 Disemba 2018 lililounda Kanuni ya Mawasiliano ya Kielektroniki ya Ulaya (OJ L 321, 17.12.2018, uk. 36).